**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA BARAZA LA UDHIBITI WA MFUMO WA UTOAJI LESENI ZA BIASHARA, NAM. 13 YA 2013 NA KUTUNGA SHERIA YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA UTOAJI LESENI ZA BIASHARA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Matumizi.

3. Ufafanuzi.

### SEHEMU YA PILI
### UANZISHWAJI WA MAMLAKA

4. Uanzishwaji wa Mamlaka.

5. Muhuri na nembo ya Mamlaka.

6. Malengo ya Mamlaka.

7. Kazi za Mamlaka.

8. Uwezo wa Mamlaka.

### SEHEMU YA TATU
### USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAMLAKA

9. Uanzishwaji na muundo wa Bodi

10. Sifa za Mwenyekiti.

11. Katibu wa Bodi.

12 Kazi za Bodi.

13. Uwezo wa Bodi.

14. Mwenendo wa Bodi.

15. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

16. Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

17. Idara, vitengo na divisheni.

18. Wafanyakazi wa Mamlaka.

**SEHEMU YA NNE**
**MISINGI YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA LESENI ZA BIASHARA**

19. Misingi ya utoaji wa leseni, vibali, huduma na ruhusa nyengine.

20. Uanzishwaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine mpya.

21. Uidhinishwaji wa utoaji wa leseni, vibali, huduma na ruhusa nyengine.

22. Orodha ya mamlaka za leseni.

23. Wajibu wa kutoa muongozo na msaada.

24. Ushughulikiaji wa maombi na malalamiko.

25. Daftari la Kumbukumbu la Taifa la Leseni za Biashara.

26. Misingi ya usawa.

27. Misingi ya uwiano.

28. Haki ya kusikilizwa.

29. Notisi.

30. Haki ya kupata taarifa.

31. Zuio na kukataliwa haki ya kupata taarifa.

32. Maelezo ya uamuzi.

**SEHEMU YA TANO**
**TARATIBU ZA LESENI, VIBALI, HUDUMA AU RUHUSA NYENGINE**

33. Taratibu za maombi.

34. Vigezo na masharti ya leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

35. Mazingatio ya maombi.

36. Kuhudhuria kwa muombaji au mwakilishi wake.

37. Wajibu wa muombaji leseni.

38. Utoaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

39. Athari ya leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

40. Ada na tozo.

41. Uhamishaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

42. Daftari la kumbukumbu la maombi na uamuzi.

43. Kusimamishwa na kufutwa kwa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

44. Wakaguzi.

45. Kinga kwa mkaguzi.

46. Rufaa.

**SEHEMU YA SITA**
**MASHARTI YA FEDHA**

47. Fedha na rasilimali za Mamlaka.

48. Bajeti.

49. Hesabu na ukaguzi.

50. Ufunguaji wa hesabu za benki.

51. Uwezo wa kuwekeza.

52. Ripoti ya Utekelezaji wa Mwaka.

**SEHEMU YA SABA**
**MAKOSA NA ADHABU**

53. Makosa na adhabu.

54. Kumaliza makosa.

**SEHEMU YA NANE**
**MASHARTI MENGINEYO**

55. Ada ya udhibiti.

56. Kinga ya kutokuwajibika binafsi.

57. Miongozo.

58. Kanuni.

59. Kufuta na kubakiza.

**JADWELI**

**SHERIA NAM. 1 YA 2025**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

..........12 Machi.........., 2025

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA BARAZA LA UDHIBITI WA MFUMO WA UTOAJI LESENI ZA BIASHARA, NAM. 13 YA 2013 NA KUTUNGA SHERIA YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA UTOAJI LESENI ZA BIASHARA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Utoaji Leseni za Biashara Zanzibar, 2025 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika kwa madhumuni ya kusimamia na kudhibiti mamlaka zote za leseni zinazofanya kazi Zanzibar.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"biashara" inajumuisha aina yoyote ya shughuli za kibiashara, taaluma na kazi;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria hii;

"Daftari la Kumbukumbu la Taifa la Leseni za Biashara" maana yake ni Daftari la Kumbukumbu la Taifa la Leseni za Biashara liloanzishwa chini ya kifungu cha 25 cha Sheria hii;

"leseni" maana yake ni ruhusa halali kutoka kwa mamlaka za leseni ya kufanya shughuli za biashara au taaluma kwa mujibu wa masharti ya sheria yoyote husika na inajumuisha kibali, huduma na ruhusa nyengine yoyote;

"mamlaka ya leseni" maana yake ni chombo chenye mamlaka ya kisheria ya kutoa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine yoyote Zanzibar;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Utoaji Leseni za Biashara iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Mkaguzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 44 cha Sheria hii;

"Mfumo wa Taifa wa Kimtandao wa Usimamizi wa Biashara" maana yake ni mfumo unaoruhusu maombi ya leseni mtandaoni, ubadilishanaji wa taarifa na ufuatiliaji wa mamlaka za leseni;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Serikali za Mitaa" ina maana kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Nam. 7 ya 2014;

"shughuli za kibiashara" ni utoaji wa bidhaa au huduma kwa kubadilishana au kufanya malipo;

"Wakala" maana yake ni mtu ambaye anafanya kazi au anasimamia masuala ya biashara kwa niaba ya mtu mwengine; na

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na biashara

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI WA MAMLAKA

Uanzishwaji wa Mamlaka.

4.-(1) Kunaanzishwa Mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Utoaji Leseni za Biashara na ufupisho wake utakuwa ni "BLRA".

(2) Mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye urithi wa kuendelea, muhuri wake na kwa jina lake, kwa mujibu wa sheria, kitakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua na kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba au miamala yoyote;

(d) kukopa kiwango chochote cha fedha kutoka katika taasisi yoyote ya fedha, na

(e) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo lolote ambalo linaweza kutekelezwa au kufanywa na chombo kinachojitegemea.

Muhuri na nembo ya Mamlaka.

5.-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Mamlaka katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Mamlaka katika waraka wowote yatathibitishwa kwa saini ya Mkurugenzi Mkuu au afisa mwengine yeyote wa Mamlaka aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Waraka wowote utakaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Mamlaka utawekwa muhuri wa Mamlaka na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Malengo ya Mamlaka.

6. Malengo ya Mamlaka yatakuwa ni:

(a) kuimarisha na kurahisisha mfumo wa usimamizi na udhibiti wa leseni za Biashara Zanzibar; na

(b) kudhibiti na kusimamia mamlaka za leseni na kuondoa vikwazo katika kufanya biashara.

Kazi za Mamlaka.

7-(1) Kazi za Mamlaka zitakuwa ni:

(a) kudhibiti na kusimamia mamlaka za leseni kufuata masharti ya Sheria hii;

(b) kupitia masharti yote yaliyopo na yanayopendekezwa katika utoaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine na kutoa maelekezo kwa mamlaka ya leseni husika kufanya marekebisho ya masharti hayo;

(c) kuanzisha, kutekeleza na kuendesha Mfumo wa Taifa wa Biashara na Mfumo wa Taifa wa Kimtandao wa Usimamizi wa Biashara;

(d) kudhibiti, kufuatilia na kuzitaka mamlaka za leseni kutumia mifumo inayotolewa na Mamlaka katika utoaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine;

(e) kupendekeza kwa Serikali juu ya mambo yanayotokana na mapitio yaliyofanywa chini ya aya ya (b) ya kifungu hiki;

(f) kufanya tathmini na ufuatiliaji kuhusiana na utoaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine kwa ajili ya kuweka mazingira rafiki ya biashara; na

(g) kutekeleza kazi nyengine yoyote kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

(2) Mamlaka, katika kutekeleza kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itashauriana na wadau kutoka katika taaluma husika na jamii ya wafanyabiashara.

Uwezo wa Mamlaka.

**8**. Mamlaka itakuwa na uwezo wa:

(a) kutoa maelekezo kwa mamlaka za leseni kuhusiana na utoaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine;

(b) kuandaa na kupitia viwango vya ada na tozo za leseni, vibali, huduma na ruhusa nyengine;

(c) kuzikagua mamlaka za leseni ili kuhakikisha zinafuata masharti ya Sheria hii;

(d) kutathmini uwezo wa watumishi, muundo wa taasisi na mfumo wa utendaji wa mamlaka za leseni;

(e) kupendekeza aina mpya za leseni, vibali, huduma na ruhusa nyengine itakayofaa kutolewa na mamlaka za leseni;

(f) kusitisha au kufuta leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine kutoka kwa mamlaka za leseni;

(g) kusimamisha leseni za aina moja zinazotolewa na mamlaka mbili tofauti; na

(h) kuzitaka mamlaka za leseni kutoa taarifa zinazohusiana na leseni, kibali, huduma, ruhusa nyengine, ada au tozo nyengine kama itakavyohitaji katika kutekeleza kazi zake.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAMLAKA

Uanzishwaji na muundo wa Bodi.

9.-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu;

(c) Mkurugenzi anayehusika na Uratibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(d) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(e) wajumbe watatu kila mmoja kutoka:

(i) Wizara inayohusika na fedha;

(ii) Wizara inayohusika na biashara; na

(iii) Jumuiya ya Wafanyabiashara Zanzibar;

(2) Wajumbe waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1)(d) na (e) ya kifungu hiki watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia sifa, uzoefu na jinsia zao.

Sifa za Mwenyekiti.

**10**. Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo.

(a) ana angalau shahada ya kwanza kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba katika nafasi ya uongozi; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu.

Katibu wa Bodi.

**11**.-(1) Bodi itamteua mfanyakazi wa Mamlaka kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria au mwenye sifa ya kuwa katibu wa shirika kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali; na

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika utumishi wa umma;

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi, na:

(a) kwa kushauriana na Mwenyekiti, ataandaa ajenda za vikao vya Bodi;

(b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(c) atatunza kumbukumbu sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(d) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe;

(e) atafanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Kazi za Bodi.

**12**. Bodi itakuwa na kazi, za:

(a) kuandaa, kufuatilia, kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa masuala yote yanayohusiana na usimamizi wa Mamlaka;

(b) kumshauri Waziri juu ya masuala yanayohusiana na mfumo wa utoaji leseni za biashara na mamlaka za leseni,

(c) kuamua mikakati na sera zinazosimamia uendeshaji wa Mamlaka; na

(d) kutekeleza kazi nyengine yoyote chini ya Sheria hii.

Uwezo wa Bodi.

**13**. Bodi, katika kutekeleza kazi zake, itakuwa na uwezo wa:

(a) kumuelekeza Mkurugenzi Mkuu kuipatia Bodi taarifa yoyote, ripoti, nyaraka nyengine ambazo Bodi itaona ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu yake;

(b) kuanzisha Kanuni za Wafanyakazi na Kanuni za Fedha za Mamlaka;

(c) kupitia na kuidhinisha sera, mpango kazi, mpango mkakati, bajeti na ripoti za Mamlaka;

(d) kutoa maelekezo halali kwa Mkurugenzi Mkuu kuhusiana na usimamizi na utekelezaji wa Mamlaka;

(e) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mfanyakazi wa Mamlaka kwa mujibu wa sheria;

(f) kuidhinisha muundo wa utumishi wa Mamlaka kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011;

(g) kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam.2 ya 2011, kuweka vigezo na masharti ya utumishi, mishahara na posho ikijumuisha stahiki nyengine yoyote kwa wafanyakazi wa Mamlaka;

(h) kuidhinisha ada na tozo baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa Mamlaka; na

(i) kuajiri wafanyakazi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

Mwenendo wa Bodi.

**14.** Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

**15.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba; na

(c) uadilifu wa hali ya juu

Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

**16.**-(1) Mkurugenzi Mkuu atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka na atawajibika kusimamia utekelezaji wa kazi za kila siku za Mamlaka na atawajibika kwa Bodi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu:

(a) atasimamia utekelezaji wa malengo, sera na kanuni za Mamlaka na kutoa taarifa kwa Bodi;

(b) atasimamia fedha na mali za Mamlaka kwa mujibu wa sheria husika;

(c) atasimamia na kudhibiti nidhamu za wafanyakazi wa Mamlaka;

(d) atatunza na kusimamia taarifa zitakazoingizwa katika Daftari la Kumbukumbu la Taifa la Leseni za Biashara la mamlaka za leseni.

(e) atashughulikia maombi yanayowasilishwa katika Mamlaka kutoka mamlaka za leseni; na

(f) atatekeleza kazi nyengine yoyote muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria hii kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Idara, vitengo na divisheni.

**17.**-(1)Mamlaka inaweza kuanzisha idara, vitengo na divisheni kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

(2) Wakuu wa idara na vitengo watateuliwa na Bodi kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(3) Wakuu wa divisheni watateuliwa na Mkurugenzi Mkuu kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(4) Wakuu wa idara, vitengo na divisheni watawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu.

Wafanyakazi wa Mamlaka.

**18.** Kutakuwa na wafanyakazi wa Mamlaka ambao wataajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam.2 ya 2011.

## SEHEMU YA NNE
## MISINGI YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA LESENI ZA BIASHARA

Misingi ya utoaji wa leseni, vibali, huduma na ruhusa nyengine.

**19.**-(1) Mamlaka za leseni zitazingatia misingi ifuatayo:

(a) taratibu na vigezo vinavyolingana na vilivyorahisi vya utoaji wa leseni, vibali, huduma na ruhusa nyengine;

(b) mfumo wa leseni uliowazi, uliosawa, uliobora, wenye ufanisi na wenye gharama nafuu;

(c) kuhakikisha kwamba huduma inayotolewa inalingana na ada inayotozwa;

(d) malipo ya ada maalumu na ada zilizowekwa wazi na kutozwa kwa madhumuni pekee ya kulipia gharama za usimamizi kuhusiana na leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine;

(e) kuhakikisha uhalali wa leseni, kibali, huduma au ruhusa nyengine;

(f) ubadilishanaji wa taarifa husika miongoni mwa mamlaka za utoaji wa leseni ili kurahisisha utoaji wa leseni, vibali, huduma na ruhusa nyengine;

(g) leseni, kibali, huduma au ruhusa nyengine zitakuwa kwa madhumuni ya kudhibiti na kusimamia biashara na siyo kwa ajili ya kuweka vikwazo katika ushindani;

(h) leseni zitakuwa halali kwa kipindi cha muda wa miezi kumi na mbiii au zaidi;

(i) vibali vitakuwa halali kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili;

(j) kuepusha hali ya urasimu na ukiritimba; na

(k) kuweka ulinzi wa taarifa na usiri kibiashara wa taarifa zote zinazokusanywa katika mfumo isipokuwa endapo utoaji wa taarifa unahitajika kisheria.

(2) Mamlaka za leseni zitahakikisha kwamba masharti ya kuwa na leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine hayatosababisha au kupelekea:

(a) madhara kwa maslahi ya umma;

(b) madhara kwa usalama wa taifa;

(c) ukiukwaji wa miongozo ya kimataifa;

(d) ukiukaji wa masharti ya udhibiti wa ubora, ithibati ya ubora usalama au afya na usafi;

(e) kutokuwa na uweledi wa taaluma;

(f) biashara isiyo halali au ushindani usio halali ambao hauwezi kuzuiwa ipasavyo kwa taratibu nyengine za kisheria;

(g) kupungua kwa maliasili, urithi wa utamaduni au matumizi yasiyo endelevu; au

(h) sababu nyengine zozote zinazokubalika.

(3) Masharti yaliyowekwa yanayohusiana na leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine yatatumika tu kwa biashara ambayo inafanywa au kupendekezwa kufanywa.

Uanzishwaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine mpya.

**20**.-(1) Mamlaka ya leseni inayokusudia kuanzisha leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine mpya:

(a) itatoa taarifa kwa maandishi ya nia hiyo kwa Mkurugenzi Mkuu;

(b) itafanya mashauriano na wadau ambao wataathirika na hatua iliyokusudiwa; na

(c) itawasilisha kwa Mkurugenzi Mkuu ripoti ya mashauriano ya wadau pamoja na tathmini ya athari za shughuli za biashara inayopendekezwa kutumika.

(2) Mkurugenzi Mkuu atafanya mapitio ya ripoti iliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1)(c) cha kifungu hiki na endapo masharti hayakidhi vigezo vilivyowekwa katika kifungu cha 19 cha Sheria hii, atatoa mapendekezo kwa mamlaka za leseni.

Uidhinishwaji wa utoaji wa leseni, vibali, huduma na ruhusa nyengine.

**21**. Mamlaka ya leseni yoyote inayokusudia kutoa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine, itaomba idhini kwa Mamlaka kwa mujibu wa taratibu zitakazoelezwa katika kanuni.

Orodha ya mamlaka za leseni

**22**.-(1) Mamlaka, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, itatoa orodha ya mamlaka za leseni zilizoidhinishwa kutoa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

(2) Mamlaka yoyote ya leseni ambayo haijajumuishwa katika orodha iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, haitatoa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine ya kuanzisha biashara au kujihusisha na miamala ya kibiashara.

Wajibu wa kutoa muongozo na msaada.

**23**.-(1) Mamlaka ya leseni itakuwa na wajibu wa kutoa muongozo na msaada kwa waombaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

(2) Endapo mamlaka ya leseni itapokea maombi ya maandishi kuhusiana na jambo lililo nje ya uwezo wake inaweza kumuelekeza muombaji kwa mamlaka ya utoaji wa leseni husika.

Ushughulikiaji wa maombi na malalamiko.

**24**.-(1) Maombi ya leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine yaliyofanywa kwa mamlaka za leseni yatashughulikiwa haraka iwezekanavyo na katika mazingira yoyote haitozidi siku thelathini za kazi.

(2) Endapo lalamiko limepelekwa kwa mamlaka za leseni kuhusiana na maombi ya leseni, kibali, huduma au ruhusa nyengine litaamuliwa ndani ya siku saba za kazi.

Daftari la Kumbukumbu la Taifa la Leseni za Biashara

**25**.-(1) Mamlaka itaanzisha na kutunza Daftari la Kumbukumbu la Taifa la Leseni za Biashara la mamlaka zote za leseni na leseni, vibali, huduma na ruhusa nyengine zinazotolewa Zanzibar.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kuelezea katika kanuni:

(a) taarifa zinazopaswa kukusanywa na kurikodiwa na Mamlaka kuhusiana na leseni, vibali, huduma na ruhusa nyengine;

(b) taarifa zinazopaswa kujumuishwa katika Daftari la Kumbukumbu la Taifa la Leseni za Biashara au daftari jengine la kumbukumbu;

(c) namna ya kutunza Daftari la Kumbukumbu la Taifa la Leseni za Biashara;

(d) ukaguzi wa Daftari la Kumbukumbu la Taifa la Leseni za Biashara; na

(e) uchapishaji wa taarifa zilizopo katika Daftari la Kumbukumbu la Taifa la Leseni za Biashara

Misingi ya usawa

26.-(1) Mamlaka ya leseni, katika kushughulikia maombi, itahakikisha na kuzingatia misingi ya usawa.

(2) Muombaji hatabaguliwa kwa misingi ya ukabila, asili, jinsia, rangi, utaifa, dini, imani ya kisiasa, familia, ulemavu au mambo mengine yanayofanana na hayo.

Misingi ya uwiano.

27. Mamlaka ya leseni itazingatia misingi ya uwiano katika kutoa uamuzi na inaweza kutoa uamuzi mgumu endapo madhumuni halali yaliyokusudiwa hayawezikufikiwa.

Haki ya kusikilizwa.

28.-(1) Muombaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine au mkata rufaa atapewa fursa ya kuelezea maoni yake juu ya ombi au rufaa kabla mamlaka ya leseni kufikia uamuzi wa mwisho.

(2) Endapo muombaji au mkata rufaa amepewa haki ya kueleza maoni yake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mamlaka ya leseni itamtaarifu muombaji au mkata rufaa au mwakilishi wake ndani ya siku kumi na nne za kazi ambapo ombi au rufaa itaamuliwa.

Notisi.

29.-(1) Endapo mamlaka ya leseni haijaridhika na jambo lolote linalohusiana na:

(a) maombi yaliyofanywa ya leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine; au

(b) biashara inayofanywa,

mamlaka ya leseni:

(i) kwa upande wa aya ya (a) itampa muombaji notisi ya kukataliwa ndani ya siku tatu za kazi na sababu za kukataliwa huko; au

(ii) kwa upande wa aya ya (b) itampa muombaji notisi ya kusudio la kusimamisha biashara kwa mtu husika ndani ya siku tatu za kazi na sababu za kusimamishwa huko.

Haki ya kupata taarifa.

30.-(1) Muombaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine au mkata rufaa atakuwa na haki ya kupata taarifa kuhusiana na ombi au rufaa.

(2) Endapo mamlaka ya leseni imefikia uamuzi wa ombi la taarifa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itamtaarifu muombaji au mkata rufaa ndani ya siku tatu za kazi.

(3) Masharti ya kifungu hiki hayatatumika kwa upelelezi na uendeshaji wa shauri la jinai, isipokuwa kwamba mshitakiwa katika shauri hilo anaweza kuomba jalada la shauri baada ya shauri kusitishwa au kukamilika.

Zuio na kukataliwa haki ya kupata taarifa.

31.-(1) Mamlaka ya leseni inaweza kuzuia upatikanaji wa taarifa kwa muombaji au mkata rufaa kutokana na maslahi ya umma au binafsi.

(2) Endapo mamlaka ya leseni imekataa kumpa taarifa muombaji au mkata rufaa, itamtaarifu muombaji au mkata rufaa kwa maandishi pamoja na sababu za kukataa huko.

(3) Kwa kuzingatia sheria zinazotumika, zuio la kupata taarifa linaweza kulalamikiwa kwa mamlaka yenye uwezo ndani ya siku saba za kazi.

Maelezo ya uamuzi.

32.-(1) Mamlaka ya leseni itahakikisha kwamba katika kufanya uamuzi, rejea zitafanywa kwa mujibu wa taratibu za kisheria ambazo uamuzi wa mamlaka ya leseni imefikia.

(2) Endapo uamuzi wa mamlaka ya leseni umefikiwa maelezo ya uamuzi yatajumuisha maoni muhimu yanayoamua matokeo ya maelezo na maelezo mafupi ya maeneo muhimu yanayopelekea uamuzi katika shauri.

## SEHEMU YA TANO
## TARATIBU ZA LESENI, VIBALI, HUDUMA NA RUHUSA NYENGINE

Taratibu za maombi.

33.-(1) Ombi kwa ajili ya kutoa, kufuta, kuhuisha au kuhaulisha leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine kwa mamlaka ya leseni litakuwa kwa namna kama itakavyoelezwa na mamlaka ya leseni husika.

(2) Ombi lililotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, litakamilika na kuweka saini na muombaji au wakala wake na litawasilishwa kwa mamlaka ya leseni pamoja na, pale itakapohitaji:

(a) nakala ya cheti cha usajili wa biashara kilichothibitishwa au nambari ya usajili wa biashara;

(b) uthibitisho wa uanachama wa taasisi ya taaluma husika na mafunzo au jumuiya;

(c) Cheti cha ithibati cha Polisi; na

(d) Nambari ya Utambulisho ya Mlipakodi.

(3) Mamlaka ya leseni inaweza kukubali uwasilishwaji wa maombi chini ya kifungu hiki kwa njia ya kielektroniki na kuambatanishwa na saini ya kielektroniki.

Vigezo na masharti ya leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

34. Endapo zipo aina maalumu za shughuli ambazo zinazohusiana na leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine zinazotolewa na mamlaka ya leseni na zinahitaji vigezo na masharti maalumu ya kitaalamu, vigezo na masharti hayo maalumu ya kitaalamu yataelezwa katika sheria husika.

Mazingatio ya maombi.

35.-(1) Mamlaka ya leseni, kabla ya kutoa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine, itawasalisha ombi kwa Afisa anayehusika na leseni husika kwa mazingatio.

(2) Endapo mamlaka ya leseni imejiridhisha kwamba muombaji ametimiza vigezo vyote husika, itatoa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine kwa muombaji.

Kuhudhuria kwa muombaji au mwakilishi wake.

36.-(1) Mamlaka ya leseni inaweza, endapo itahusika, itatoa taarifa ya kuhudhuria katika kikao kwa muombaji mpya au mwakilishi wake ambapo ombi linakusudiwa kuzingatiwa.

(2) Mamlaka ya leseni inaweza kukataa kuzingatia ombi ikiwa muombaji au mwakilishi wake, bila ya taarifa yoyote ya awali, hatahudhuria kikao ambacho ombi linakusudiwa kuzingatiwa.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, muombaji anayehuisha au kuhaulisha moja kwa moja leseni, kibali, huduma au ruhusa nyengine au anayefanya ombi kuhusiana na tawi jipya la ofisi hahitaji kuhudhuria kikao ambacho ombi lake linakusudiwa kuzingatiwa isipokuwa kama muombaji amepewa taarifa na mamlaka ya leseni kuhudhuria.

Wajibu wa muombaji leseni.

**37**.-(1) Muombaji atakuwa na wajibu wa kupata leseni nyengine yoyote, kibali, huduma na ruhusa nyengine inayohitajika chini ya sheria nyengine yoyote.

(2) Mamlaka ya leseni itasaidia maombi kwa kutoa taarifa zote husika ili kuwawezesha waombaji kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na taarifa zitakuwemo katika muongozo unaohitajika chini ya kifungu cha 23 cha Sheria hii.

Utoaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

**38**.-(1) Mamlaka ya leseni itatoa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine kwa kila muombaji ambaye amefuata masharti ya sheria husika ndani ya siku tatu za kazi.

(2) Mamlaka ya leseni, itakapohitajika, itatoa nakala ya leseni, kibali na ruhusa nyengine yoyote iliyotolewa chini ya kifungu hiki na itaithibitisha nakala hiyo kuwa ni nakala halisi ya leseni, kibali na ruhusa nyengine.

Athari ya leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

**39**.-(1) Leseni mpya, kibali, huduma na ruhusa nyengine itaanza kutumika itakapotolewa na mamlaka ya leseni.

(2) Endapo ombi limefanywa kwa ajili ya kuhuisha leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine kuhusiana na ombi lililofanywa itaendelea kutumika hadi ombi la kuhuisha litakapokubaliwa na mamlaka ya leseni au ikiwa ombi la kuhuisha limekataliwa, hadi muda ambao rufaa iliyokatwa imeisha muda wake, au rufaa imefutwa au imeamuliwa.

Ada na tozo.

**40**. Mamlaka itatangaza ada na tozo za leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine inayotolewa na mamlaka za leseni katika namna inayofaa.

Uhamishaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

**41**.-(1) Mamlaka ya leseni inaweza, baada ya kupokea ombi, kuhamisha kwa mmiliki mpya, au warithi au waliyopewa mali kisheria na marehemu mwenye leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine iliyotolewa kuhusiana na eneo au biashara kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usajili wa Biashara, Nam. 12 ya 2012

(2) Leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine iliyohamishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki itaanza kutumika hadi kumaliza muda wake na itashikiliwa kwa mujibu wa masharti ambayo ilitolewa awali.

(3) Endapo leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine imehamishiwa chini ya kifungu hiki kwa mtu yeyote, mamlaka ya leseni, baada ya kulipa ada inayostahiki, itaidhinisha notisi ya uhamisho wa leseni, kibali, huduma au ruhusu nyengine.

(4) Leseni, kibali, huduma au ruhusa nyengine iliyotolewa kwa watu binafsi kwa ujuzi wao binafsi, sifa, uzoefu au uwezo wengine hauwezi kuhamishwa.

Daftari la kumbukumbu la maombi na uamuzi.

**42**.-(1) Mamlaka ya leseni itaweka daftari la kumbukumbu la maombi na uamuzi kwa ajili ya leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

(2) Daftari la kumbukumbu la maombi na uamuzi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, litakaguliwa na Mamlaka.

Kusimamishwa na kufutwa kwa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

**43**.-(1) Mamlaka ya leseni inaweza kusimamisha au kufuta leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine kwa sababu zifuatazo:

(a) mmiliki hafai na hastahiki tena kumiliki leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine;

(b) mmiliki amekiuka vigezo na masharti yanayotumika kwa leseni hiyo, kibali, huduma na ruhusa nyengine;

(c) matumizi ya maeneo ambayo leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine ni tishio kwa afya au usalama wa umma;

(d) maeneo ambayo leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine inatumika hayakidhi tena viwango vilivyowekwa na sheria husika; au

(e) mmiliki au wakala wake amemkatalia mkaguzi aliyeidhinishwa kuingia au kutoa ushirikiano kwa mkaguzi kama inavyohitajika na Sheria hii au sheria nyengine inayotumika kwa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine.

(2) Mamlaka ya leseni inaweza, katika kuzingatia lalamiko linalotokana na usimamishwaji au ufuatwaji chini ya kifungu hiki, kuzingatia ukiukwaji wa maadili kwa upande wa mmiliki wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine ikiwa inapelekea au haipelekei ukiukwaji wa masharti ya sheria husika..

(3) Endapo mamlaka ya leseni itatoa amri ya kusimamisha leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine, usimamishaji huo hautatekelezwa hadi kumalizika kwa muda ambao mmiliki anaweza kukata rufaa au ikiwa rufaa imekatwa, hadi imeachwa kusikilizwa au imeamuliwa.

(4) Masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki hayatatumika endapo usimamishwaji wa haraka utahitajika kwa maslahi ya afya na usalama kwa ajili ya watu wengine au umma.

(5) Muda wa kusimamisha leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine chini ya kifungu hiki utakuwa muda maalumu usiozidi mwaka mmoja.

Wakaguzi.

44.-(1) Mamlaka au mamlaka ya leseni inaweza kuteua wakaguzi ili kuhakikisha masharti ya Sheria hii na sheria nyengine zinazohusiana na biashara, leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine yanafuatwa.

(2) Mamlaka au mamlaka ya leseni itatoa kitambulisho kwa mkaguzi na mkaguzi atakionesha kitambulisho hicho wakati wa kuingia katika eneo lolote ambalo linatakiwa kukaguliwa au kwa mtu yeyote ili kupata taarifa zinazohusiana na leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine chini ya masharti ya Sheria hii na sheria nyengine zinazohusika.

(3) Mkaguzi anaweza:

(a) kuingia na kukagua, kwa wakati unaofaa, eneo lolote ambalo biashara inayohusiana na leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine inafanyika;

(b) kufanya uchunguzi au ukaguzi wa vifaa na huduma zinazotolewa;

(c) kuchukua hati halisi au nakala ikijumuisha hati za kielektroniki; na

(d) kutoa amri ya kufunga biashara endapo biashara imekiuka Sheria hii au sheria nyengine yoyote husika au endapo inahatarisha usalama wa umma.

(4) Mkaguzi hatotoa taarifa yoyote aliyoipata wakati wa ukaguzi au uchunguzi isipokuwa ikihitajika na mahakama au kutoa taarifa kama sehemu ya kazi yake

(5) Mkaguzi ambaye ana maslahi binafsi, kifedha au ya moja kwa moja ambayo yanaweza kuathiri mazingatio ya jambo lolote mbele yake hatokagua au kuchunguza jambo hilo.

(6) Mkaguzi yeyote aliyetajwa chini ya kifungu hiki ambaye anatumia vibaya nafasi yake, anasababisha uharibifu, anakamata mali au anatoa taarifa yoyote kinyume na sheria wakati wa kutekeleza majukumu yake ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania au kifungo kwa muda usiopungua mwaka moja na usiozidi miaka mitatu au vyote faini na kifungo.

Kinga kwa mkaguzi.

**45**. Mkaguzi, wakati wa kutekeleza uwezo aliyopewa na Sheria hii au sheria nyengine husika, hatowajibika kwa jambo lolote alilofanya au aliloacha kulifanya ikiwa jambo hilo limefanywa au limeachwa kufanywa kwa nia njema.

Rufaa.

**46**.-(1) Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa mamlaka ya leseni anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo kwa mujibu wa sheria husika ya mamlaka ya leseni.

(2) Sababu za rufaa zitakuwa moja kati ya zifuatazo:

(a) uamuzi umetokana na taarifa zisizojitosheleza au zisizo sahihi kuhusiana na maelezo;

(b) uamuzi umetokana na mazingira ambayo yalibadilika kwa kiasi kikubwa kiuhalisia;

(c) mamlaka ya leseni imekiuka taratibu za kisheria;

(d) mamlaka ya leseni imeenda kinyume na misingi ya haki;

(e) uamuzi ulikuwa nje ya uwezo wa mamlaka ya leseni; au

(f) mamlaka ya leseni ilikiuka masharti ya Sheria hii au sheria nyengine husika;

(3) Rufaa itawasilishwa ndani ya siku ishirini na moja za kazi kuanzia tarehe ya taarifa ya uamuzi kwa mtu ambaye anahusika.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na rasilimali za Mamlaka.

**47**.-(1) Fedha na rasilimali za Mamlaka zitajumuisha:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha zinazopokelewa na Mamlaka kwa huduma zinazotolewa na Mamlaka;

(c) ruzuku halali, zawadi, michango, misaada au mikopo kama Mamlaka itakavyopokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote;

(d) ada na tozo zinazokusanywa chini ya Sheria hii;

(e) mapato yanayotokana na uwekezaji utakaofanywa na Mamlaka; na

(f) fedha nyengine zozote zinazoweza kupatikana kihalali na Mamlaka.

(2) Mamlaka itabakiza asilimia ishirini na tano ya mapato yanayokusanywa kutokana na vyanzo mbali mbali kuhusiana na utekelezaji wa kazi zake.

Bajeti.

**48**.-(1) Mkurugenzi Mkuu, kila mwaka wa fedha, atawasilisha kwa Bodi kwa ajili ya majadiliano na mapendekezo ya makadirio ya kina ya mapato na matumizi ya Mamlaka kwa mwaka ujao wa fedha.

(2) Baada ya kujadiliwa na kupendekezwa na Bodi, bajeti ya Mamlaka itachukuliwa kuwa ni sehemu ya bajeti ya Wizara.

(3) Makadirio ya mapato na matumizi ya Mamlaka yataandaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016 na miongozo mengine yoyote kama itakavyotolewa na Serikali kila baada ya muda.

(4) Mkurugenzi Mkuu atahakikisha kwamba, malipo yote yanayofanywa kutokana na fedha za Mamlaka yanafanywa kwa usahihi na yanaidhinishwa ipasavyo na udhibiti wa kutosha unadumishwa juu ya mali na madeni ya Mamlaka.

Hesabu na ukaguzi.

**49**.-(1) Mamlaka itaweka na kutunza kwa usahihi vitabu vya hesabu ambavyo vinajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha.

(2) Taarifa za fedha za mwaka za Mamlaka zitakaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016 na sheria za fedha nyengine husika.

Ufunguaji wa hesabu za benki.

**50**. Mamlaka, kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016, itafungua hesabu ya benki kwa ajili ya utekelezaji mzuri ya kazi zake chini ya Sheria hii.

Uwezo wa kuwekeza.

**51**. Mamlaka itakuwa na uwezo wa kuwekeza fedha zake katika uwekezaji ambao utakuwa wa faida, salama na halali kwa mujibu wa sheria husika.

Ripoti ya utekelezaji wa mwaka.

**52**.-(1) Mkurugenzi Mkuu, ndani ya miezi mitatu baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha, ataandaa na kuwasilisha kwa Waziri ripoti ya utekelezaji ya mwaka kuhusiana na mwaka huo wa fedha.

(2) Waziri ataiwasilisha nakala ya ripoti ya utekelezaji ya mwaka ya Mamlaka mbele ya Baraza la Wawakilishi ndani ya miezi miwili au katika Mkutano unaofuata wa Baraza la Wawakilishi, baada ya kupokea ripoti hiyo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu.

**53**.-(1) Mamlaka ya leseni ambayo:

(a) itatoza ada au tozo bila kutoa huduma iliyokusudiwa;

(b) itatoza ada au tozo bila ya kuwa na sheria inayosimamia ambayo imetoa kazi au uwezo;

(c) itashindwa kusimamia kazi zinazohusiana na utoaji wa leseni, kibali, huduma na ruhusa nyengine chini ya Sheria hii;

(d) itamzuia afisa wa Mamlaka katika kutekeleza kazi za Mamlaka chini ya Sheria hii; au

(d) itashindwa kufuata masharti ya Sheria hii,

imetenda kosa na ikitiwa hatiani, italipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Hamsini za Kitanzania.

(2) Endapo mamlaka ya leseni imetenda kosa chini ya Sheria hii na kosa hilo limethibitishwa kuwa limefanywa kwa ridhaa au ushirikiano wa, au kuhusishwa na uzembe kwa upande wa Afisa Mtendaji Mkuu au afisa aliyeidhinishwa wa mamlaka ya leseni atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani ataadhibiwa na sheria husika watakuwa na hatia ya kosa hilo na watashtakiwa na kuadhibiwa ipasavyo.

Kumaliza makosa.

**54**.-(1) Mkurugenzi Mkuu anaweza kumaliza kosa lililofanywa na mamlaka ya leseni chini ya Sheria hii au kanuni zake kwa kumtaka kulipa faini isiyopungua nusu ya faini iliyoainishwa kwa kosa hilo, iwapo mamlaka ya leseni au mkaguzi:

(a) amekubali kwamba ametenda kosa;

(b) atalipa malipo yote ya msingi chini ya Sheria hii.

(2) Taratibu zinazohusiana na kumaliza kosa zitaainishwa katika kanuni.

(3) Kumaliza kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hautochukuliwa kama ni hatia kwa kosa linaloshukiwa kufanywa na isipokuwa kwamba malipo ya msingi yamelipwa yote, hakutokuwa na mashtaka kwa kosa linaloshughulikiwa ambalo litafunguliwa au kuendelezwa.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

Ada ya udhibiti.

**55**. Mamlaka, kwa kushauriana na mamlaka ya leseni itatoza ada ya udhibiti kwa mujibu wa taratibu zitakazoainishwa katika kanuni.

Kinga ya kutoku-wajibika binafsi.

**56**. Wafanyakazi wa Mamlaka hawatowajibika kwa jambo lolote walilofanya au waliloacha kulifanya ikiwa jambo hilo limefanywa au limeachwa kufanywa kwa nia njema katika kutekeleza kazi na uwezo wa Mamlaka chini ya Sheria hii.

Miongozo.

**57**. Mamlaka inaweza kutoa miongozo kwa ajili ya utendaji bora wa kazi zake chini ya Sheria hii.

Kanuni.

**58**. Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**59**.-(1) Sheria ya Baraza la Udhibiti wa Mfumo wa Utoaji wa Leseni za Biashara, Nam. 13 ya 2013 inafutwa.

(2) Bila ya kujali ufutaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa, litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI

---

## MWENENDO WA BODI
**[Chini ya kifungu cha 14]**

---

Makamu Mwenyekiti.

**1**. Wajumbe wa Bodi watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Muda wa wajumbe.

**2**. Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Bodi.

**3**.-(1) Bodi itakutana kikawaida kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana muda wowote itakapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti na ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

**4**. Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wataunda akidi katika kikao chochote cha Bodi.

Uamuzi wa Bodi.

**5**. Uamuzi wa Bodi utafanywa kwa maafikiano, endapo hakuna maafikiano, uamuzi utafanywa kwa kupiga kura na endapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Taratibu za vikao.

**6**. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itajipangia taratibu zake wenyewe kuhusiana na vikao na uendeshaji mzuri wa shughuli zake ikijumuisha Kamati za Bodi.

Mjumbe mualikwa.

**7**. Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria majadiliano yoyote ya kikao cha Bodi kama mtaalamu lakini mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kumbu-kumbu za vikao vya Bodi.

**8**. Kumbukumbu za vikao vya Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

Kukasimu kazi za Bodi.

**9.** Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi maalumu kama itakavyoona inafaa.

Kamati za Bodi.

**10.**-(1) Bodi inaweza, itakavyoona inafaa kwa ajili ya kutekelezaji wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati za Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji bora wa kazi.

Kusita kuwa mjumbe.

**11.** Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya afya ya kimwili au kiakili;

(d) ikiwa atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyomteua mjumbe huyo;

(e) ikiwa atasimamishwa na Waziri akishindwa kutimiza matarajio ya Mamlaka; au

(f) amefariki.

Kubainisha maslahi.

**12.**-(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kuzingatiwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada ya kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha:

(a) hatohudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya uamuzi; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya uamuzi.

Posho la wajumbe wa Bodi.

**13.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 12 Februari, 2025.

..............................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar***